The Regulator
Januari – Machi 2026

Jarida la kila robo mwaka la Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

Na 3-2025/2026



NAKALA YA BURE

# Mageuzi Makubwa Sekta ya Utangazaji Tanzania

ISO 9001:2015 CERTIFIED
www.tcra.go.tz

ISSN: 0856-8030

# Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

## Dira

Jamii iliyowezeshwa na huduma za mawasiliano jumuishi na endelevu.

## Dhima

Kusimamia huduma za mawasiliano kwa ustawi wa Jamii ya Watanzania.

## Wajibu

Wajibu wa Mamlaka ya Udhibiti Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni kusimamia sekta ya mawasiliano na kielektroni na posta kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania Namba 12 ya mwaka 2003.

## Tunu Kuu

### 1. WELEDI

Tunatekeleza majukumu yetu kwa kutoa huduma bora bila upendeleo tukizingatia maadili na heshima stahiki kwa wadau wetu.

### 2. UBUNIFU

Tunazingatia ubunifu na kuendelea kuboresha na kushughulikia masuala ya usimamizi kwa kuzingatia yanayotokea kwenye mazingira ya teknolojia ambayo yanabadilika kila wakati.

### 3. UTENDAJI WA PAMOJA

Tunaamini katika nguvu ya ziada inayotokana na utendaji kazi wa pamoja na ushirikiano ili kufikia malengo ya pamoja, kwa kutambua kuwa mawasiliano kwa njia ya ufanisi na inayojenga ni muhimu ili kujenga mazingira yanayochangia ushirikiano kwenye shughuli zetu.

### 4. WEPESI KUBADILIKA

Tumejiandaa kubadilika, kuendana na mabadiliko na kukabiliana na kuendana na yanayojitokeza, teknolojia na changamoto za usimamizi kwenye sekta ya mawasiliano.

**Anwani ya ofisi za uhariri.**


Mawasiliano Towers, Na. 20 Barabara ya

Sam Nujoma, S.L.P 474,Postikodi: 14414 Dar es Salaam. Simu: +255 784558270, +255 784558271. baruapepe: regulator.magazine@tcra.go.tz; dg@tcra.go.tz. Toleo la kidijiti linapatikana mtandaoni kwenye: https://www.tcra.go.tz/documents/ the-regulator

ISSN: 0856-8030

# Kampeni ya Usalama Mtandaoni


## Hatari za kumsajilia mtu mwingine laini ya Simu



Kusajili laini ya simu kwa niaba ya mtu mwingine kuna athari kubwa zinazoweza kukusababishia wewe na wengine madhara kisheria, kifedha na kibinafsi.

1. *Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta Kuhusu Usajili wa Laini za Simu zinakataza kutumika kitambulisho cha mtu mwingine kusajili laini ya simu.*
2. *Taarifa na alama au data nyingine ya utambulisho ya mtu atakayekuwa akitumia laini hiyo lazima ziunganishwe moja kwa moja na laini ya simu.*
3. *Adhabu kali kwa kusajili laini ya simu kwa kutumia kitambulisho chako kwa niaba ya mtu mwingine ni pamoja na shilingi milioni tano kwa mtu binafsi na shilingi milioni 50 kwa kampuni au kifungo cha hadi miezi 12.*
4. *Mtoa huduma wa laini uliyoisajili atahusisha mawasiliano yote yanayofanyika kwa laini hiyo na kitambulisho chako na hivyo utawajibika kwa matumizi mabaya ya laini hiyo. Hii ni pamoja na ulaghai na utapeli kwa njia ya simu, wizi wa utambulisho na uhalifu wa mtandaoni.*
5. *Unapomsajilia mtu mwingine laini ya simu, unachukua dhamana ya kisheria kwa matendo yote yanayofanyika kwa kutumia laini hiyo. Mtu huyo akifanya uhalifu kama vile utapeli au miamala haramu, uchunguzi utafuatilia rekodi za usajili hadi kukufikia uliyesajili laini husika.*
6. *Kumsajilia laini mtu mwingine pia kuna athari kubwa kwa faragha yako – unahatarisha faragha ya data zako. Data zako za kibayometria hutumika, ikiwamo alama za vidole au utambuzi wa sura, kulingana na mfumo unaotumika. Data hizi ni za kipekee na zinalenga kukulinda wewe pamoja na mtandao wa mawasiliano dhidi ya ulaghai.*
7. *Shughuli za udanganyifu zinazohusisha laini za simu zimeongezeka na wahalifu mara nyingi wanatafuta njia za kukwepa sheria. Ikiwa laini ya simu iliyosajiliwa kwa jina lako inahusishwa na miamala ya udanganyifu, matokeo yake yanaweza kuwa mabaya: sio tu kukumbana na adhabu za kisheria, bali kupata hasara za kifedha kutokana na matumizi mabaya ya huduma za pesa kwa njia ya simu au vitendo vya utapeli.*
8. *Unapomsajilia mtu mwingine laini ya simu, unapoteza uwezo wa kufuatilia jinsi namba hiyo inavyotumiwa na unawajibika kwa matumizi yake – kwa shughuli halali au zisizo halali. Matendo yasiyo ya kimaadili au ya kihalifu yatakayofanyika kwa kutumia laini hiyo bado yatakuwa yakihusishwa nawe, hata kama hukujua au kushiriki moja kwa moja.*
9. *Kanuni zimeainisha utaratibu wa kuwasajilia watoto au watu ambao kwa sababu zinazokubalika hawawezi kutumia vitambulisho vyao kusajili laini.*
10. *10.Tafadhali wasiliana na mtoa huduma wako au TCRA, kupitia namba ya bure 0800008272 kwa maelezo zaidi.*

**Baki salama!**



ISSN: 0856-8030

# Regulator linatolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

## Wajibu na kazi za TCRA kwa mujibu wa Sheria Na. 12 ya mwaka 2003 iliyoianzisha ni:

1. *Kukuza ushindani bora na uchumi wenye tija.*
2. *Kulinda maslahi ya watumiaji.*
3. *Kulinda mitaji ya Watoa Huduma wenye ufanisi.*
4. *Kukuza upatikanaji wa huduma zinazosimamiwa kwa watumiaji wote wakiwamo wenye kipato kidogo, walioko vijijini na watumiaji walio na walioko katika mazingira magumu.*
5. *Kuimarisha Elimu kwa Umma, uelewa na ufahamu wa huduma zinazosimamiwa na TCRA, ikiwa ni pamoja na:*
    i. *Haki na wajibu wa watumiaji na watoa huduma zinazosimamiwa;*
    ii. *Namna ya kuwasilisha malalamiko na migogoro na utaratibu wa utatuzi wake; na*
    iii. *Kazi na majukumu ya Mamlaka kwa kuzingatia umuhimu wa kulinda na kutunza mazingira.*

## TCRA inaendeleza upatikanaji wa huduma zinazosimamiwa kupitia utaratibu wa leseni za huduma za mawasiliano. Inasimamia masharti ya leseni na ya kanuni zinazotokana na Sheria zinazohusu mawasiliano. Mamlaka inatoa leseni za huduma za mawasiliano na pia kufuta inapobidi kwa kuzingatia ubora wa utoaji huduma za Mawasiliano, Posta na Utangazaji. Vilevile inasimamia utendaji wa watoa huduma katika sekta, ikiwa ni pamoja na

a. *Kuweka na kusimamia viwango kwa watoa huduma*
b. *Kudhibiti ubora wa utoaji na usambazaji wa huduma.*
c. *Kushughulikia malalamiko na kusuluhisha migongano na migogoro ndani ya sekta.*
d. *Kushirikiana na wasimamizi wa mawasiliano wa nchi nyingine ili kuandaa mikakati itakayosaidia kuboresha utoaji huduma nchini.*
e. *Kutekeleza mikataba ya kimataifa katika sekta ya mawasiliano*
f. *Kuiwakilisha Tanzania kwenye mashirika ya kimataifa ya mawasiliano.*
g. *Kutekeleza majukumu mengine yatakayopangwa kwa mujibu wa sheria za nchi.*


## Bodi ya Uhariri

**Mwenyekiti**

Mhandisi. Mwesigwa Felician

**Katibu**

Mr. Rolf Kibaja

**Wajumbe**

Bw. Semu Mwakyanjala (Coordinator)

Dkt. Philip Filikunjombe

Bw. Peter Lyimo

Bw. Abel John

Bw. Robin Ulikaye

Bw. Vitalia Kidabulo


Bw. Alpha Wawa

**Mhariri Uzalishaji**

Bw. Isaac Mruma

**Msanifu**

Bw. Jackson Mkufya

ISSN: 0856-8030

# Barua ya Mhariri

## Msukumo mpya kuimarisha utangazaji

Makala nyingi kwenye toleo hili zinaangazia juhudi mbalimbali za kuimarisha sekta ya utangazaji nchini, kuanzia uwekaji miunbombinu wezeshi hadi ufikishaji wa maudhui bora yanayokidhi mahitaji ya hadhira.

Tunapitia juhudi za Serikali kuhakikisha kuwa miundombinu ya mawasiliano inayojengwa na kutumika inawezesha huduma za utangazaji kufikia wananchi wote. Miongoni mwa mipango hiyo ni uwepo wa setilaiti ya kwanza ya Tanzania,ambayo itasaidia kufikisha mawimbi ya utangazaji katika maeneo ya mbali na maeneo yenye changamoto za kijiografia,ikiwemo maeneo ya milimani na mabondeni.



Utangazaji unaendelea kuwa chanzo muhimu cha habari,elimu na burudani kwa Watanzania wengi, ambapo zaidi ya asilimia 85 ya wananchi wanategemea maudhui ya redio. Ufikiaji wa hadhira umeboreshwa.


Redio zaidi ziko hewani, zikiwahakikishia Watanzania uanuai wa maudhui. Kufikia Machi 2026 kulikuwa na redio 266 na televisheni za kawaida 73. Redio na televisheni mtandaoni zilikuwa 12 na 221, mtawalia.

TCRA imealika maombi ya masafa yanayopatikana katika baadhi ya mikoa kwenye bendi ya masafa ya 87.5 hadi 108 MHz kwa matangazo ya redio ya FM. Masafa hayo yakitumika yataongeza ueneaji wa redio ya FM miongoni mwa watu na kijiografia. TCRA pia imetoa zabuni za watoa huduma za kurusha matangazo ya redio kwenye mikoa mitano chini ya mfumo wa redio kidijitali unaotarajiwa kuanza mwaka huu.

Vile vile tunachambua mapendekezo ya utafiti wa uliofanywa na TCRA kuhusu mbinu za kuboresha utangazaji. Aidha, tunazo dondoo kutoka Mkakati wa miaka 10 wa TCRA wa Usimamizi wa Masafa. Mkakati huo, utakaotekelezwa hadi mwaka wa fedha 2034/2035 ni dira ya usimamizi madhubuti wa masafa ya masafa. Madhumuni ni kuongeza kuenea kwa huduma za utangazaji kwa watu na kijiografia.

Takwimu za mawasiliano za robo mwaka ya Januari-Machi 2026 zinaonesha ukuaji wa kasi wa matumizi ya data mitandaoni ndani ya miaka mitano. Matumizi yalipaa kwa asilimia 700 kati ya Machi 2021 na Machi mwaka huu, na kwa asilimia 15 kutoka Desemba 2025.

Hata hivyo, bidhaa za posta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi zilipungua kwa asilimia 85 kati ya Machi 2021 na Machi mwaka huu na kwa asilimia 4 kutoka Desemba.





ISSN: 0856-8030

# YALIYOMO




**05** Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu



**07** Mageuzi Utangazaji Tanzania



**10** Mikoa mitano kufikiwa na redio kidijitali



**12** Utafiti kuboresha mahitaji ya utangazaji



**13** TCRA yalenga mabadiliko, ushirikishaji



**15** Takwimu za robo mwaka

ISSN: 0856-8030



# Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu

## Mpango mkakati mpya TCRA walenga mabadiliko, ushirikishaji

Toleo hili linaambatana na uzinduzi wa Mpango Mkakati wa tano wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania utakaotekelezwa kati ya mwaka wa fedha 2026/27 na 2030/31. Mpango huu unalenga kuhakikisha huduma za mawasiliano zinapatikana kwa wote kwa njia jumuishi, shindani na endelevu zinazowezesha mabadiliko ya kidijitali na maendeleo ya taifa.

Mpango huu umeandaliwa ili kushughulikia vipaumbele vya kitaifa kwa lengo la kuleta mabadiliko ya kidijitali. Hii ni sehemu ya Dira ya TCRA ya kuwezesha jamii kwa huduma za mawasiliano jumuishi na endelevu kupitia miundombinu ya mawasiliano, programu tumizi na huduma dhabiti.



TCRA imesawanisha shughuli zake na malengo ya maendeleo ya taifa, pamoja na misimamo ya kikanda na kimataifa. Masuala ya maendeleo kitaifa, kikanda na kimataifa yanavyoiongoza TCRA ni pamoja na yale kwenye Misingi ya Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali Tanzania 2024 – 2034, Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2050, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala (2025-2030) na sera za kisekta.

Mpango huu wa kimkakati umezingatia sera muhimu za kitaifa, ikiwemo sera ya Taifa ya TEHAMA, Sera ya Taifa ya Habari na Utangazaji na Sera ya Taifa ya Posta. Sera hizi zinalenga kuharakisha mageuzi ya kidijitali na kuongeza fursa zaidi katika sekta ya mawasiliano ya simu na intaneti, utangazaji na posta.

Katika ngazi ya kimataifa, mpango huu unaunga mkono utekelezaji wa Malengo ya Kimataifa ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2030, Ajenda ya Afrika 2063. Dira ya kuimarisha mabadiliko ya kidijitali katika sekta ya TEHAMA barani Afrika na namna zinavyotambua nguvu ya mabadiliko ya TEHAMA ni miongoni mwa vichochezi vingine vinavyoongoza TCRA.



Aidha, TCRA imeweka mkazo katika mazingira endelevu kwa kuzingatia misingi ya ESG (Environmental, Social and Governance) ili kukuza ukuaji wa sekta ya mawasiliano unaowajibika na endelevu kimazingira.

Malengo ya Kimkakati kwa miaka mitano (5) ijayo yanasisitiza ukuzaji miundombinu inayostahimili mabadiliko, na iliyo endelevu na salama. Malengo mengine ni kuendeleza upatikanaji wa huduma za mawasiliano zinazosimamiwa kwa gharama wanazomudu watumiaji.



TCRA inaamini kuwa mustakabali wa Sekta ya Mawasiliano utachangiwa na mazingira madhubuti, hasa teknolojia zinazoibukia na matumizi yake. Mpango huo unalenga kupanua na kuendeleza miundombinu na huduma za mawasiliano ya kasi, kukuza maudhui ya ndani, kushirikisha wadau na kuhakikisha uendelevu wa kitaasisi.

Hii itawezesha upatikanaji na matumizi ya huduma za kidijiti katika mazingira jumuishi, ubunifu na usalama kwenye mawasiliano, hivyo kuchangia mabadiliko ya kitaifa na maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

Kwa utekelezaji mzuri wa Mpango huu, TCRA inasisitiza azma na kuwezesha watumishi wake kuwa na afya njema na kujenga uwezo wao kutekeleza majukumu yao na kukidhi matarajio ya umma, huku ikitoa usimamizi thabiti wa Sekta ya Mawasiliano ambao inazingatia mabadiliko ya kiteknolojia.



ISSN: 0856-8030

# Mtizamo

# Mipango kushughulikia vikwazo vya ujumuishaji wa kifedha

Na Mwandishi wa Regulator

Wawakilishi wa wadau wakuu katika huduma za kifedha kidijitali wamependekeza njia za kukuza ufikiaji wa huduma za kifedha za kidijitali kwa watu wengi, kulinda watumiaji dhidi ya ulaghai na kuendeleza ujasiriamali wezeshi.

Mapendekezo hayo yalifikiwa katika mkutano wa hivi karibuni wa Kikundi Kazi cha Kiufundi cha Sekta Ndogo ya Fedha (TWG) jijini Dodoma. Mkutano huo uliitishwa na Wizara ya Fedha, mratibu wa TWG, kujadili utekelezaji wa Mpango Kazi wa Sekta Ndogo ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2025/26.

Majadiliano yalihusu kuiimarisha sekta ndogo ya fedha kidijittali, nafasi ya mitandao ya kijamii na majukwaa ya kidijitali na kama njia za kufanikisha utoaji wa mikopo na ufadhili wa vifaa vya mawasiliano.

Ajenda zingine zilikuwa miundombinu ya kidijitali na uelewa wa masuala ya kidijitali, masuala ya fedha kwa kilimo uwezeshaji wa wajasiriamali na wawekezaji wa ndani ya Tanzania.

Wataalam hao walibaini kuwa kuna ongezeko la njia za kidijitali zinazoimarisha utoaji wa huduma. Hata hivyo, walibaini kuwa gharama za baadhi ya huduma za kidijitali zilikuwa juu na hivyo kuwa kikwazo kwa taasisi nyingi ndogo za fedha.

Walitoa wito wa kuchukukiwa hatua zinazolenga kupunguza gharama, na hivyo kusukuma mifumo ya kidijitali jumuishi na

mageuzi katika sekta ndogo. Hii pia itaendeleza lengo pana la kufikia uchumi usio na fedha Tanzania.




**Masuala makuu yaliyojitokeza**

1. *Kupatikana kwa Tanzania ya kidijitali kikamilifu kimsingi inategemea mambo mengi. Baadhi ni miundombinu ya kidijitali, hasa upatikanaji, na uchukuliwaji kwa matumizi. Mengine ni kutegemewa kwa muunganisho wa mawasiliano ya kasi pamoja na upatikanaji wa vifaa vya bei nafuu kuwezesha ufikiaji wa maana wa huduma za kidijitali.*

2. *Kuna ongezeko la idadi ya mifumo ya kidijitali isiyo na leseni na akaunti za mitandao ya kijamii zinazotoa huduma za mikopo moja kwa moja kwa umma. Watoa huduma hizi wengi wa aina hii hutumia mapengo katika ujuzi wa kidijitali na kifedha. Wanawahadaa watu kwa vitendo vya ulaghai na miradi ya ulaghai ya mikopo..*

3. *Katika muktadha wa mabadiliko ya haraka ya kidijitali, ufuatiliaji na udhibiti wa shughuli kama hizo umezidi kuwa mgumu, hasa pale ambapo ufahamu wa umma unabaki kuwa mdogo.*

4. *Licha ya maendeleo makubwa katika uwekaji miundombinu, uelewa mdogo wa masula ya kidijitali bado ni changamoto kubwa. Katika baadhi ya matukio, mifumo ya kidijitali inatumiwa vibaya kwa shughuli za ulaghai na usambazaji wa taarifa potofu, badala ya kutumika kama zana za maendeleo ya kijamii na kiuchumi.*

5. *Mkakati muhimu unahitajika kupunguza hali hii ni kuimarisha ujuzi wa kidijitali na wa masuala ya kifedha.*

6. *Wizara ya Fedha itaimarisha ushirikiano na TCRA na Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ili kutekeleza programu zilizoratibiwa za kujenga uwezo ili kuimarisha ujuzi wa kifedha wa kidijitali na kukuza upatikanaji jumuishi wa huduma za kifedha za kidijitali. TCRA inatoa leseni kwa kampuni za mkononi na pia inatoa namba na misimbo kwa watoa huduma kidijitali. BOT inasimamia sekta ya fedha. Taasisi hizi zinashirikiana kwenye masuala kadhaa.*

7. *Programu za kuongeza uelewa zinapaswa kuunganishwa katika hatua za awali za elimu ili kuhakikisha kwamba watoto na vijana wanakuza ufahamu na ujuzi unaohitajika ili kutumia huduma za kifedha za kidijitali kwa uwajibikaji.*

8. *TCRA inaendelea kutekeleza kampeni za uhamasishaji na mipango ya kukuza ubunifu wa TEHAMA kwa ushirikishwaji wa kidijitali katika uchumi.*

9. *Ulaghai kwenye majukwaa ya WhatsApp unapaswa kuzuiwa. Wataalamu hao walibainisha kuwa hata pale namba inayojihusisha na shughuli za ulaghai kwenye mitandao ya simu iliporipotiwa au kuzimwa katika ngazi ya mtandao husika wa simu, inaweza kuendelea kufanya kazi kupitia WhatsApp na kuwalenga waathirika wengine.*

# Mageuzi Makubwa Utangazaji Tanzania

## Na Mwandishi wa Regulator

Tanzania inabadilisha sekta yake ya utangazaji kwa kupanua huduma hadi maeneo ya vijijini na yasiyohudumiwa vya kutosha, kuanzisha utangazaji wa sauti za kidijitali katika miji yenye uhaba wa masafa katika bendi ya FM, na kukuza utengenezaji wa maudhui ya ndani.

Kwa kuwa Watanzania wengi wanaendelea kutumia huduma za utangazaji kama chanzo muhimu cha habari na burudani, redio inaendelea kuwa jukwaa linalotumika sana, huku takriban asilimia 85 ya watazamaji wa utangazaji wakiitegemea. Watoa huduma za utangazaji, kupitia vyombo vya kawaida na vya mtandaoni, wana jukumu muhimu katika kuhudumia hadhira ya utangazaji kote nchini. Hadhira hii inajumuisha wasikilizaji wa redio, watazamaji wa televisheni, na watazamaji wa mitandao ya kijamii.

Serikali, kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (USCAF) na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania,inatekeleza programu kadhaa zinazolenga kuboresha na kupanua miundombinu ya utangazaji kupitia ujenzi wa minara, ujenzi wa tovuti, pamoja na ununuzi wa vifaa vya utangazaji. Kufikia Machi 2026, Mfuko umetoa ruzuku kwa ajili ya ujenzi wa minara thelathini na mbili (32) ya mawasiliano.

Serikali imechukua hatua kuweka miundombinu ya utangazaji, ikiwa ni pamoja na kujenga minara vijijini ili kufikisha matangazo maeneo yenye ugumu kijiografia kufika mawimbi ya redio na televisheni.

Ujenzi huu unaratibiwa na UCSAF. Miradi iliyotekelezwa na Mfuko huo imeanishwa hapa chini..

*Hali ya utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa miundombinu ya utangazaji kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kufikia Machi 2026*

UCSAF imetekeleza miradi ya kuongeza wigo wa usikivu wa redio husussan katika maeneo ya vijijini na yenye huduma hafifu. Minara thelathini na mbili (32) imepatiwa ruzuku, ambapo kumi na moja (11) imekamilika na ishirini na moja (21) iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Miradi kumi (10) ya ujenzi wa minara ya redio jamii imetekelezwa katika hatua mbalimbali katika mikoa ya Dodoma, Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Pwani, Tanga, Lindi, Simiyu, Arusha na Morogoro. Miradi saba kati ya hiyo imekamilika.

Studio mbili (2) zimeboreshwa katika mikoa ya Dodoma na Arusha ili kuimarisha ubora wa uzalishaji na usambazaji wa maudhui ya utangazaji.

Hatua hizi zimeelezwa kuchangia kuongezeka kwa upatikanaji wa taarifa kwa wananchi, kuimarisha maudhui ya kijamii kupitia redio na kupunguza pengo la huduma za utangazaji katika maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara.

**Chanzo:** *Wasilisho la UCSAF kwenye mkutano wa mwaka wa wadau wa utangazaji, Dodoma, Februari 2026.*

Mkongo wa Kitaifa wa TEHAMA (NICTBB) umepanuliwa na umeunganisha wilaya themanini na tano (85) kufikia Machi 2026. Upanuzi huu una athari chanya kwa gharama za watoa huduma za utangazaji na data.

Miundombinu na huduma mpya za utangazaji vinatarajiwa kukidhi mahitaji na matarajio yanayobadilika ya raia wake katika enzi ya kidijitali.

Vile vile, TCRA inatekeleza Mkakati wa Usimamizi wa Spektra (Spectrum) wa miaka 10, uliozinduliwa Septemba 2024, ili kuongoza usimamizi bora wa wigo wa masafa ya redio hadi 2034/2035. Mamlaka inafanya kazi ya kuongeza upenyaji wa huduma za utangazaji na kupanua wigo wa kijiografia.


Kufikia Machi 2026, upenyaji wa mawimbi ya FM ulifikia asilimia themanini na tano ya watu Tanzania. Katika hatua ya kuongeza ueneaji na kuongeza utofauti wa maudhui, TCRA imewaalika watoa huduma za utangazaji wa redio kuomba huduma katika mikoa ishirini (20) na kushindana kwa masafa mia mbili sabini na nne (274) ya FM ifikapo tarehe 1 Juni mwaka huu.

Mkakati wa Usimamizi wa Spektra pia unasimamia masafa ya redio kwa teknolojia za satelaiti na simu. Ugawaji mzuri wa masafa ya redio kwa huduma za utangazaji huhakikisha upana wa kutosha wa matangazo ya televisheni na redio duniani. Bendi za masafa ya redio zilizotengwa kwa redio ya FM Tanzania ni kuanzia 87.5 hadi 108 MHz.

Bendi za huduma za utangazaji wa televisheni duniani ziko katika wigo wa 470 hadi 694 MHz huku bendi za 174 hadi 230 MHz na 525 hadi 1605 kHz zikitumika kwa Utangazaji wa Sauti ya Dijitali (DSB) nchini Tanzania, kwa kutumia viwango vya T-DAB na DRM.

DSB inatarajiwa kuongeza ubora wa huduma za utangazaji huku ikitumia vyema rasilimali za masafa ya redio zinazopatikana na kutatua changamoto ya uhaba wa masafa ya redio katika miji mikubwa.

| Mkoa | Idadi ya redio | Idadi ya Masafa yanayosubiri kutolewa |
|---|---|---|
| Arusha | 18 | 4 |
| DSM | 27 | |
| Dodoma | 13 | |
| Geita | 3 | |
| Iringa | 10 | 13 |
| Kagera | 14 | 5 |
| Katavi | 4 | 21 |
| Kigoma | 8 | 9 |
| Kilimanjaro | 16 | 6 |
| Lindi | 2 | 18 |
| Manyara | 6 | 12 |
| Mara | 5 | 15 |
| Mbeya | 22 | 2 |
| Morogoro | 23 | 14 |
| Mtwara | 13 | 25 |
| Lindi/Mtwara | 22 | |
| Mwanza | 18 | 23 |
| Njombe | 8 | |
| Pwani/Coast | 5 | 25 |
| Rukwa | 4 | 17 |
| Ruvuma | 10 | 6 |
| Shinyanga | 8 | 25 |
| Simiyu | 3 | 14 |
| Singida | 1 | |
| Songwe | 1 | 13 |
| Tabora | 5 | 3 |
| Tanga | 11 | |



ISSN: 0856-8030

TCRA imekuwa ikishughulikia maendeleo katika teknolojia za utangazaji na changamoto za sekta ndogo.

Mwaka wa 2024, TCRA ilifanya utafiti uliopitia mfumo wa Kisheria na usimamizi wa sekta ndogo ya utangazaji ya Tanzania. Utafiti huo ulipendekeza mapitio ya kanuni ili kuunda uwanja wa usawa zaidi kwa kuzingatia kuenea kwa maudhui kupitia majukwaa yanayotegemea intaneti. Kulikuwa pia na mapendekezo kuhusu uzingatiaji wa viwango vya utangazaji na masuala ya maudhui ya ndani.

Utafiti huo pia ulipendekeza mfumo mpya wa leseni kwa sekta ya utangazaji, ikijumuisha makundi ya leseni, muda na ada. Leseni inapaswa kutegemea "sehemu za uwepo" badala ya maeneo ya utawala.

Mfumo wa sasa una leseni za kitaifa, kikanda, wilaya na jamii kwa maudhui yasiyolipiwa na hadhira. Leseni za maudhui ya kulipia ni za huduma za kitaifa na wilaya.

Vipengele muhimu vya ripoti na mapendekezo yake vimewasilishwa hapa chini.

*Baadhi ya mambo kwenye ripoti ya utafiti kuhusu mfumo wa usimamizi wa utangazaji wa Tanzania.*

Maendeleo katika sekta ya utangazaji ya Tanzania yanahitaji mfumo mpya wa usimamizi/udhibiti.

Utafiti huo ulibainisha udhaifu katika mnyororo wa huduma. Huduma za televisheni, redio, na utoaji maudhui mtandaoni zimeunda mifumo mipya ya biashara. Mfumo wa utangazaji uliokuwepo hauendelei. Majukwaa ya kidijitali yasiyo na leseni yaliyoendeshwa pamoja na vyombo vya habari vya jadi, ambavyo vililipa ada na vililazimika kuzingatia upendeleo wa maudhui.

Watangazaji wa vyombo vya kawaida wanashindwa kushindana na majukwaa ya mitandaoni (OTT) yanayofadhiliwa na matangazo. Majukwaa haya yanafanya kazi bila gharama za usimamizi au majukumu ya maudhui. Hii inasababisha kuwepo maudhui yasiyongatia viwango. Rejea ukurasa wa 9:.

Vituo vya redio na televisheni vya jadi vya kawaida vyenye leseni vinashindana na majukwaa ya kidijitali yasiyo na leseni katika hali ambayo haioneshi usawa. Vinakosa mapato ya matangazo ambayo hapo awali yaliviwezesha kujiendesha na kujikimu.

Baadhi ya watangazaji hawakuwa na mipango ya biashara, na kusababisha utendaji duni na kushindwa kulipa ada za usimamizi, mishahara ya wafanyakazi, na majukumu mengine.

Baadhi ya waendeshaji walio na leseni hawakuwa wameanza shughuli ndani ya kipindi kilichowekwa ingawaje walikuwa na vipindi muhimu ambavyo vingeweza kutumika kukidhi mahitaji yanayoongezeka na kupanua wigo wa habari.

Kuna haja ya uingiliaji kati wa haraka ili kuepuka Tanzania kupoteza uzalishaji wa maudhui ya ndani, kuzuia anguko la vyombo vya habari vya jadi, na kuruhusu majukwaa ya kigeni kutawala bila kuchangia malengo ya maendeleo ya ndani.



Mshauri huyo alibainisha namna ambavyo utangazaji wa jadi, huduma za sauti na video mtandaoni, na masoko ya matangazo vimeunganishwa.

Kanuni za utangazaji za Tanzania zinapaswa kupitiwa upya ili kushughulikia mienendo ya soko lililobadilika kidijitali.

Mshauri huyo pia alipendekeza vigezo vipya vya leseni kwa mifumo tofauti ya biashara na mifumo ya usimamizi ili kuwezesha ushindani wa haki kati ya majukwaa ya jadi na ya mtandaoni.

Walipendekeza kanuni za maudhui zilizounganishwa katika njia zote za uwasilishaji wa maudhui.

Kunapaswa kuwa na mikakati ya maudhui ya ndani ambayo inasawazisha mienendo ya soko na malengo ya kitamaduni.

Muundo wa ada za leseni na wigo unapaswa kuwa endelevu kwa waendeshaji ili kuwahakikishia uendelevu kiuchumi, huku wakizalisha mapato yatakayochangia shughuli za usimamizi.

TCRA imepitia ada za leseni za huduma za utangazaji. Imepunguza ada za huduma za maudhui mtandaoni na kuanzisha kundi jipya la leseni la "Watoa Huduma za Maudhui ya Mtandaoni Wanaoanza". Leseni hiyo inatoa kipindi cha mwaka mmoja bure kama motisha na baada ya hapo watalipa ada za masharti nafuu. Lengo ni kusaidia makampuni mapya na kukuza maendeleo ya maudhui ya ndani.

**Chanzo:** *https://cenerva.com/articles/transforming-tanzanias-broadcasting-landscape/*





ISSN: 0856-8030





**Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), zimeweka vigezo na mahitaji yafuatayo ya maudhui, ambayo yanatumika tu kwa watoa huduma za utangazaji wa redio na televisheni za kawaida zinazorusha maudhui yasiyolipiwa.**



1. *Kuzingatia muda wa vipindi. Wanatakuwa kutoa vipindi na maudhui ya rika zote, wakiwemo watoto, kati ya saa 11 alfajiri na saa 6 usiku. Kuanzia saa sita usiku hadi saa 11 alfajiri wanaweza kutoa maudhui yanayofaa watu wazima tu.*
2. *Kutoa maudhui mbalimbali. Programu zinapaswa kuakisi utamaduni, mahitaji, na matarajio ya Watanzania. Zinapaswa pia kujumuisha tamthilia, makala za zamani, na programu za watoto zinazoakisi mada za taifa na utambulisho wa kitamaduni.*
3. *Kutenga muda wa kutosha kwa habari. Lazima wawasilishe habari kila siku, kwa pamoja, kwa angalau dakika 90.*
4. *Kurusha programu za elimu. Watoa huduma lazima wahakikishe kwamba angalau asilimia mbili (2%) ya mpangilio wao ya kila siku ya maudhui ni ya kielimu. Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (EPOCA) inaitaka TCRA kutengeneza sheria kwa ajili ya masharti ya maudhui ya kielimu.*
5. *Maudhui ya ndani. Lazima wahakikishe kwamba angalau asilimia 60 (sitini) ya maudhui yao, yanayopimwa kama wastani wa kila wiki, ni ya ndani.*
6. *Kuchapisha na kuzingatia ratiba za vipindi. Wanatakiwa kuchapisha ratiba ya vipindi vyao katika gazeti la kila siku linalosambazwa sana nchini Tanzania au kwenye chaneli zao za utangazaji angalau mwezi mmoja mapema. Lazima wafuate ratiba hii isipokuwa kama wanalazimika kutangaza matukio ya moja kwa moja, ya ghafla yenye umuhimu wa kitaifa au kimataifa kupitia vipindi maalum.*

**Rejea:** *https://www.tcra.go.tz/documents/regulations*
*https://www.tcra.go.tz/documents/legislation-1*

ISSN: 0856-8030



# TCRA yachagua watoa huduma za maltipleksi (MUX) kwa redio kidijitali miji mitano

## Na Mwandishi wa Regulator

TCRA imechagua watoa huduma za maltipleksi (MUX) kwa huduma za redio kidijitali (DSB) Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Mwanza na Mbeya. Kila mmoja atakuwa na eneo moja la huduma. Watoa huduma hawa walipatikana kupitia mchakato wa ushindani wa zabuni.

Tanzania imeanzisha huduma za DSB ili kuboresha utangazaji wa redio na mawasiliano nchini. Viwango vitakavyotumika ni T-DAB na DRM.

Tofauti na utangazaji wa redio wa kawaida wa analojia, DSB inahusisha teknolojia inayochanganya mitiririko mingi ya sauti na data iliyosimbwa katika ishara moja kwa ajili ya uwasilishaji kupitia njia ya pamoja.

Huduma za maltipleksi hutumika katika utangazaji wa televisheni kidijitali mfumo wa ardhini (DTT) ambayo hutumia visimbuzi kufikisha maudhui kwa watazamaji.

DSB inatarajiwa kuongeza ubora wa utangazaji wa sauti ikilinganishwa na mfumo wa redio wa analojia.

Inatatua changamoto ya upatikanaji mdogo wa masafa ya redio, hasa katika maeneo ya mijini yenye msongamano na imepanua utangazaji wa redio kwa hadhira pana zaidi.

DSB hutoa njia mbadala yenye ufanisi zaidi wa masafa badala ya FM, yenye ubora wa sauti ulioboreshwa na urahisi zaidi wa watumiaji.

Kutumia masafa mengi huongeza matumizi ya masafa na kupunguza idadi ya visambazaji halisi. DSB inaruhusu vituo vingi vya redio kushiriki kizuizi kimoja cha masafa.

DSB itawanufaisha watangazaji, watumiaji, msimamizi/mdhibiti, serikali na wadau kwenye mnyororo wa usambazaji wa huduma za utangazaji. Hawa ni pamoja na watengenezaji wa maudhui, waendeshaji wa vituo vya utangazaji wa kidijitali na waagizaji na wauzaji wa vifaa. Rejea ukurasa wa 11.

Kwa kuanzisha DSB, Tanzania itaongeza kwa kiasi kikubwa usambazaji wa matangazo ya redio na kupanua ufikiaji wa maudhui ya sauti kote nchini.

DSB pia inafungua fursa za kusisimua kwa vituo vipya vya redio na kuweke uanuai wa njia za redio zinazopatikana. Inapanua kuboresha ufikiaji wa maudhui kote nchini.

Teknolojia ya redio za kidijitali pia inasaidia mawasiliano. Inapanua anuwai ya maudhui yanayopatikana na hutoa fursa za uzalishaji na usambazaji wa maudhui ya ubora wa juu kwa hadhira pana.

Vifaa vya DSB hubaki vikifanya kazi hata wakati miundombinu ya intaneti au ya simu inashindwa kutokana na sababu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuwa katika maeneo ya mbali.

Pia inasaidia shughuli za kiuchumi kama vile biashara, kilimo na shughuli za kibinafsi. Redio za kidijitali zinaweza kusambaza sauti na maandishi, ikiwa ni pamoja na kusambaza taarifa muhimu wakati wa majanga.

Wakulima wanaweza pia kupata masasisho ya hali ya hewa kwa wakati na taarifa muhimu, kama vile masoko na bei.

Masafa yaliyotengwa kwa DSB Tanzania ni katika bendi ya 174-230 Megahertz (MHz) na bendi ya 525-1605 Kilohertz (kHz).

TCRA imeunda na kuchapisha mahitaji ya chini ya kiufundi na vipimo kwa vifaa vya DSB.

Vipimo hivi vinakusudiwa kuwaongoza wasambazaji na wauzaji wa vifaa wanaotaka kuingiza vifaa hivi nchini Tanzania.

Vinalenga kuhakikisha ubora na utangamano na vifaa vingine vya mawasiliano vinavyotumika nchini.

Tanzania ni nchi ya kwanza barani Afrika kuwa na miongozo kuhusu DSB. Pia ni ya kwanza kuidhinisha vifaa vya DSB.

Kuanzishwa kwa DSB pia kunaifanya Tanzania kuwa ya kwanza tena katika eneo la Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika kwa mabadiliko ya utangazaji kidijitali.


Ilikuwa ya kwanza katika eneo hilo kuhamia kikamilifu kwenye utangazaji wa televisheni wa kidijitali kwa mfumo wa ardhini (DTT), baada ya kuzima mitandao ya analojia Desemba 2014, kabla ya tarehe ya mwisho ya kimataifa ya Juni 2015.

Hakuna tarehe ya mwisho ya kuhamia DSB, tofauti na uhamiaji wa DTT, ambayo ilikuwa na tarehe ya mwisho iliyowekwa na Shirika la Kimataifa wa Mawasiliano ya Simu (ITU).

DSB haitachukua nafasi ya utangazaji wa sauti wa analojia, na teknolojia hizo mbili zitakuwepo pamoja hadi soko litakapoamua mwelekeo.

Watangazaji waliopo wenye leseni wataruhusiwa kurusha matangazo kwenye mitandao ya kidijitali bila kulipa ada za ziada za usimamizi ili kuhimiza mpito kuelekea DSB.

Majaribio ya kwanza ya DSB yalifanywa Ulaya 1990. DRM ilitengenezwa 1997 nchini China ili kubadilisha bendi za masafa marefu, ya kati na mafupi kuwa za kidijitali. Mnamo 2005, modi za kawaida zilizojumuishwa zilibuniwa kwa bendi za utangazaji za masafa ya juu sana (VHF).







## Faida za DSB

1. *Matumizi bora zaidi ya wigo wa masafa.*
2. *Uwezo wa vituo vingi kutumia safa moja.*
3. *Hadhira pana zaidi ikilinganishwa na mifumo ya AM/FM.*
4. *Gharama ndogo za uendeshaji.*
5. *Gharama ndogo za uwasilishaji maudhui.*
6. *Ufanisi wa nishati.*
7. *Fursa mpya za huduma bunifu kwa watangazaji ambao wanaweza kutoa vituo vingi vipya vya redio ya kidijitali badala ya kituo kimoja cha redio cha analojia.*
8. *Kukuza uwekezaji katika huduma za maudhui kwa kuhimiza ushirikiano kwenye miundombinu kupitia waendeshaji wa huduma za maltipleksi.*
9. *Ubora wa sauti wa DAB ni wa juu na bora kuliko matangazo ya sasa ya redio ya AM na FM.*
10. *Uingiliaji mdogo wa kelele.*
11. *Huduma za kuaminika zaidi.*
12. *Urahisi kwa mtumiaji. Upatikanaji wa vituo vya redio umerahisishwa.*
13. *Faida kiuchumi kupitia fursa katika huduma za usaidizi katika mnyororo wa usambazaji. Hii ni pamoja na kutengeneza na kutayarisha maudhui, uagizaji na usambazaji wa vifaa vya utangazaji na simu. Aidha ufanisi wake wa nishati huwezesha nishati kupatikana kwa shughuli nyingine.*

ISSN: 0856-8030



# Utafiti kuboresha mahitaji ya utangazaji

TCRA inafanya utafiti wa usikivu na utazamaji wa vyombo vya utangazaji Tanzania. Utafiti huo utachambua kwa kina mwenendo wa utangazaji kwenye redio, televisheni na majukwaa ya mtandaoni kupitia simu janja, kompyuta na vifaa vingine vya kidijitali. Vilevile utazingatia makundi maalumu kama watoto na watu wenye ulemavu ili kuhakikisha uwakilishi jumuishi wa hadhira.

Ripoti ya utafiti huo itatoa taswira halisi ya utangazaji na viwango vya usikivu na masuala yanayohusiana na wasililizaji na watazamaji na wanaosoma maudhui mitandaoni. Pia unalenga kuboresha mipango ya maudhui yanayokidhi mahitaji halisi ya hadhira ya Tanzania.

Takwimu zitakazopatikana zitakuwa sahihi na za kuaminika, na zitazingatiwa katika kufanya maamuzi ya kisera, kiudhibiti na kibiashara kuhusu sekta ya utangazaji.

Unafanyika katika maeneo 706 ya utafiti wilaya zote 139 za Tanzania Bara. Utahusisha sampuli wakilishi kitaifa kwa mujibu wa itifaki za Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS). Sampuli itakuwa na watu na taasisi 7,000.

Utafiti unafanywa na taasisi iliyoshinda mchakato wa zabuni iliyotangazwa na kushindanisha watafiti wengi. Utafiti huu ni miongoni kwa tafiti zilizofanywa na TCRA.

Utafiti mwingine kuhusiana na utangazaji ulipitia mfumo wa Kisheria na Kiusimamizi wa sekta hii. Ulizingatia maendeleo ya teknolojia za utangazaji na changamoto za sekta ndogo ya utangazaji. Masuala muhimu kwenye ripoti ya utafiti huo yamechapishwa kwenye toleo hili.

Pia kumefanyika durusi kuhusu kuridhika kwa Watumiaji wa huduma na bidhaa zinazotolewa na wenye leseni za TCRA. Hii ilikusudiwa kuthibitisha viwango vya kuridhika kwa watumiaji wa huduma za mawasiliano.

Utafiti mwingine umepima viwango vya namna wateja wa TCRA wanavyoridhika na huduma zinazotolewa kwa kuzingatia utendaji unavyofanyika kama inavyoelekezewa kwenye vipimo vya ufanisi vya ISO 9001:2015 na Mkataba wa TCRA wa Huduma kwa Wateja.

Aidha kumefanyika utafiti kwenye Teknolojia zinazojitokeza. Huu umelenga kuweka mfumo wa usimamizi wa Akili Unde (AI) Tanzania.

Uamuzi wa TCRA kufanya utafiti kwenye maeneo ya kimkakati unakusudiwa kupata taarifa muhimu na uwezo wa kukabiliana kwa usahihi na masuala mapya na mabadiliko yanayojitokeza katika sekta. Utafiti pia unawezesha TCRA kusimamia kwa ufanisi sekta ya mawasiliano inayoendelea kubadilika.



ISSN: 0856-8030

# MAPYA KWENYE USIMAMIZI, SHERIA


## Mkakati TCRA wazingatia vipaumbele vya kitaifa

Mpango Mkakati mpya wa TCRA unawiana na sera za kitaifa zinazohusiana na utawala, mabadiliko ya kidijitali na usimamizi. Unalenga kuchangia juhudi za serikali za kuimarisha mifumo ya kitaasisi, kukuza uwajibikaji na kuhakikisha kufanikiwa mipango ya maendeleo ya sekta ya mawasiliano.

| Mipango, sera madhumuni na malengo | Majukumu, mchango wa TCRA |
|---|---|
| **Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2050.** Inaweka wazi mwelekeo wa kimkakati na vipaumbele vya maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika miongo mitatu ijayo. Madhumuni ni kuigeuza Tanzania kuwa jamii yenye kipato cha juu, ya viwanda, na inayojumuisha jamii yenye ubora wa juu wa maisha kwa wananchi wote ifikapo mwaka 2050. | Kukuza na kuendeleza miundombinu ya mawasiliano na kuunganisha mitandao ya mawasiliano ya kasi, kuimarisha usalama mtandaoni, ujuzi wa kidijiti, ujumuishaji, teknolojia zinazoibuka na uwezeshaji wa wafanyakazi kwa kukuza mfumo wa mawasiliano unaostahimili, wenye ufanisi na ulio jumuishi. |
| **Misingi ya Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali Tanzania 2024 – 2034.** Inalenga kuunda Uchumi wa kidijitali na wa buluu Tanzania na ambao ni jumuishi, thabiti, na wenye ushindani. Maeneo ya kipaumbele ni pamoja na miundombinu na huduma za kidijitali, utambulisho wa kidijiti, usalama wa mtandao, ujuzi wa kidijitali, mifumo ya uvumbuzi, teknolojia zinazibuka na majukwaa ya biashara mtandaoni. | TCRA inaendelea kupitia na kusasisha mfumo wake wa usimamizi ili kuendana na maendeleo ya mawasiliano duniani. Pia inakuza uwekezaji na ubora wa huduma kupitia utoaji wa leseni na kufuatilia uzingatiaji masharti na kanuni husika. TCRA pia inasimamia rasilimali za mawasiliano za taifa ili kuhakikisha zinatumika kwa ufanisi. |
| **Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala 2025-2030** Inaangazia umuhimu wa miundombinu ya mawasiliano katika kujenga na kudumisha uchumi endelevu, kuboresha hali ya maisha na kuimarisha kiwango cha maisha cha Watanzania. Pia inaainisha ahadi na vipaumbele vya maendeleo ya kijamii na kiuchumi, mabadiliko ya kidijitali, na ukuaji jumuishi. | Kuhakikisha kwamba mipango ya sekta inachangia katika kufanikisha vipaumbele vya kitaifa. Hatua zinazochukuliwa ni pamoja na kupanua na kuendeleza miundombinu ya mawasiliano ili kuboresha upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika maeneo ya pembezoni na ambayo hayajahudumiwa ipasavyo. Maeneo mengine ya kipaumbele ni uwekaji na utumiaji wa teknolojia zinazoibuka, pamoja na uhamasishaji na ujuzi wa kidijitali, uvumbuzi na kuimarisha usalama mtandaoni. |

ISSN: 0856-8030

| Plans, policies and their aims, objectives | TCRA's role, contribution |
|---|---|
| **Ajenda ya Uendelevu na Mazingira, Kijamii na Utawala (ESG). .**<br><br>Hii inalenga kukuza ukuaji wa uwajibikaji na endelevu wa mazingira wa Sekta ya Mawasiliano kwa kuhimiza matumizi ya teknolojia zinazotumia nishati na zinazotunza mazingira, kupunguza taka za kielektroniki na kuwezesha ushirikiano katika ujenzi na matumizi ya miundombinu. | TCRA itaunganisha kanuni za ESG katika mifumo yake ya usimamizi, uendeshaji, na ushirikiano wa wadau ili kuhakikisha kuwa sekta ya mawasiliano inachangia ipasavyo katika malengo ya maendeleo ya kitaifa na kimataifa. |
| **Sera ya Taifa ya TEHAMA**<br><br>Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)<br><br>inatambua jukumu muhimu la ukuzaji wa TEHAMA katika kuendesha uchumi wa kidijiti na wa bluu.<br><br>Inatoa mfumo wa kitaifa wa kutumia TEHAMA kuchangia kikamilifu katika kufikia malengo ya Tanzania ya maendeleo | TCRA imetekeleza mikakati kadhaa ambayo imewezesha kufikia malengo ya sera hii. Hii ni pamoja na mfumo madhubuti wa usimamizi wa ufanisi ambao unaendeleza ugawaji na matumizi bora ya rasilimali za mawasiliano, kuzingatia mabadiliko na maendeleo ya kiteknolojia, na kuwezesha mipango ya kuendeleza huduma za mawasiliano. |
| **Sera ya Habari na Utangazaji**<br><br>Inatoa mfumo elekezi wa mazingira wezeshi kwa ukuaji na uendelevu wa Sekta ya Utangazaji. Malengo yake ni kuweka mazingira mazuri ya ukuaji wa utangazaji, kukuza tunu za kitaifa na maadili ya kitaaluma, weledi na kujenga uwezo. | TCRA itaendelea kuimarisha viwango vya utendaji kwa maendeleo ya kisekta, haki, uanuwai katika utangazaji, kusimamia uwajibikaji na wahusika kuwa kuwajibika kwa wananchi kupitia uhamasishaji wa utangazaji wa maadili na taaluma. Inatekeleza mipango kadhaa ya kurekebisha na kuboresha utangazaji Tanzania. Tafadhali rejea makala kuu ya toleo hili. |
| **Sera ya Taifa ya Posta**<br><br>Inalenga kuanzisha huduma bora ya posta kwa wote kwa gharama nafuu. Pia inataka kuhakikisha kuwa huduma za posta zinakidhi mahitaji yanayokua ya kijamii, kiuchumi na kitamaduni na kuchangia juhudi za kupunguza umaskini. | TCRA imetekeleza kwa mafanikio mikakati kadhaa ili kuongeza kasi ya kufikia malengo ya sera hii. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuendelea toa leseni kwa wasafirishaji wa vifurushi ndani ya nchi na kimataifa na kubuni na kutatibu Mfumo wa Kitaifa wa Anwani za Makazi na Misimbo ya Posta. |






# Sekta ya Mawasiliano
Katika
**Namba**

ISSN: 0856-8030




# Matumizi data mtandaoni yapaa ila uwezo hautumiki ipasavyo

Na Mwandishi wa Regulator

Matumizi ya huduma za data mtandaoni yameongezeka kwa asilimia 700 ndani ya miaka mitano na kwa 15.3 kati ya Desemba 2025 na Machi mwaka huu ingawaje bado kuna uwezo wa kukua zaidi, ripoti ya hali ya sasa ya mawasiliano Tanzania inaonesha.

Ripoti ya Machi 2026 iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Mhandisi Peter Mwasalyanda inasema watumiaji intaneti walifikisha petabaiti 932 Machi mwaka huu kulinganisha na petabaiti 117 Machi 2021 na petabaiti 808 Desemba 2025.


Uchambuzi wa ripoti hiyo umebaini kuwa pamoja na ongezeko hilo, bado matumizi ya intaneti Tanzania yako chini. Wanaojiunga na mitandao Tanzania wanatumia asilimia 16.5 tu ya uwezo uliopo wa kuunganisha huduma ya intaneti kimataifa.




Matumizi ya intaneti

Ripoti hiyo imeeleza kuwa uwezo uliopo ni gigabaiti kwa sekunde (Gbps) 17,690 huku zinazotumika ni 2,915, hivyo kuwa na 14,775 kwa uunganishaji mpya.

"Uwepo wa uwezo wa ziada utafanikisha upatikanaji wa maudhui zaidi ya kimataifa, huduma za kuhifadhi data mtandaoni na matumizi mengine na unatoa fursa ya uwekezaji katika huduma ya intaneti ya kasi," taarifa imeeleza.




Watumiaji intaneti

| | Uwezo wa kutoka nje (Gbps) | Uwezo wa kuingia (Gbps) |
|---|---|---|
| Jumla ya uwezo | 17,690 | 17,690 |
| Uwezo unaotumika | 2,915 | 2,915 |
| Uwezo unaosubiri kutumika | 14,775 | 14,775 |

*Uwezo wa intaneti kimataifa kufikia Machi 2026*

Majukwaa haya yanatumika kwa mawasiliano, kusambaza maudhui mtandaoni na burudani. You tube inatumika zaidi kwa filamu na video na TikTok kwa video fupi za elimu na vichekesho.

Facebook ni mtandao wa jamii unaounganisha watu mbalimbali na kuwawezesha kupeana taarifa, Instagram ni maarufu kwa taarifa fupi zenye muda wa kuonekana na WhatsApp ni kwa makundi sogozi na inawezesha watumiaji simu za gharama ndogo inayotegemea data iliyolipiwa.

Kiasi cha data kwenye kompyuta na vifaa vya kielektroniki kinapimwa kwa baiti. Zikifika 100 ni kilobaiti (Kb), 1,000 ni megabaiti (Mb), milioni moja ni gigabaiti (Gb). Petabaiti (Pb) moja ni sawa na gigabaiti milioni moja.

ISSN: 0856-8030



# Leseni mpya zaongeza ueneaji huduma, matumizi

TCRA ilitoa hadi asilimia 21 ya leseni mpya kwenye makundi mbalimbali kati ya Januari na Machi mwaka huu, hivyo kupanua wigo na upatikanaji wa huduma. Miundombinu mipya imepanua upatikanaji wa huduma za intaneti na mawasiliano na kuongeza ujumuishi wa watumiaji kwenye huduma za kifedha kidijitali.

Leseni hizo mpya ni pamoja na saba za mitandao ya mawasiliano (NF), moja ya huduma za mtandao (NS) na 14 za programu tumizi za mawasiliano (AS).

Leseni za mtandao ziliongezeka kutoka 48 hadi 52. Hizi zinamruhusu mtoa huduma kumiliki miundombinu kama minara ya mawasiliano ya simu za mkononi, minara na vifaa vya kurushia matangazo ya vyombo vya utangazaji na nyaya za simu na mitambo ya mawasiliano.

Leseni za NS zinamruhusu mwenye leseni kutoa huduma za msingi za kuunganisha mitandao mbalimbali ya mawasiliano. Hizi ziliongezeka kutoka 25 hadi 26. Ingawaje mwenye leseni hii pia anaweza kuwa na leseni ya miundombinu, mfumo wa leseni unaruhusu watoa huduma kutumia miundombinu ya wengine.

Leseni ya programu tumizi inamruhusu mmiliki kuwezesha matumizi ya huduma kama za data, biashara mtandaoni na huduma nyingine za usambazaji wa mawasiliano. Hizi ziliongezeka kutoka 159 Januari hadi 173 Machi mwaka huu.

TCRA pia ilitoa vyeti vipya 65 vya matumizi ya Mifumo ya Kimataifa ya Usalama na Dharura Baharini (GMDSS). Mfumo huu unatoa taarifa za kiotomatiki za dharura na unaowezesha mawasiliano ya usalama kwa kasi wakati wa dharura baharini. Unarahisisha shughuli za uokoaji kwenye meli.

Vilevile TCRA ilitoa leseni saba mpya za huduma za maudhui ya redio za wilaya, moja kwa ajili ya huduma za redio za jamii na tano za usafirishaji wa vifurushi ndani ya nchi ndani.

Hadi Machi 2026 kulikuwa na redio ngazi ya wilaya 188, redio za mikoa 37, redio za kitaifa 14 na 20 za jumuia. Kulikuwa na televisheni za taifa za bila malipo (FTA) 21, televisheni za wilaya za FTA 21 na televisheni 51 za waya. Aidha kulikuwa na televisheni 30 za kulipia ngazi ya taifa na moja ngazi ya wilaya kufikia Machi 2026.

| Kundi la leseni | Idadi ya leseni | |
|---|---|---|
| | Desemba 2025 | Machi 2026 |
| Televisheni bila malipo (FTA) kitaifa | 21 | 21 |
| Televisheni bila malipo (FTA) ngazi ya wilaya | 21 | 21 |
| Redio kitaifa | 14 | 14 |
| Redio ngazi ya mkoa | 37 | 37 |
| Redio ngazi ya wilaya | 188 | 195 |
| Redio za jamii | 19 | 20 |
| Redio maudhui maalum kitaifa | 1 | 1 |
| Televisheni za kulipia kitaifa | 30 | 30 |
| Televisheni za kulipia wilayani | 1 | 1 |
| Idhini ya utangazaji kitaifa | 1 | 1 |
| Huduma wezeshi za maudhui kitaifa | 30 | 3 |
| Waandaaji wa maudhui ya kutoa mitandaoni | 6 | 6 |
| Blogu | 77 | 74 |
| Redio mtandao | 13 | 12 |
| Televisheni mtandao | 222 | 221 |
| Televisheni kwa njia ya waya | 55 | 51 |

*Idadi ya Leseni za Huduma za Utangazaji*

ISSN: 0856-8030




# Ukuaji pesa mtandaoni waonesha mwelekeo huduma kwa wote

Zaidi ya asilimia 72 ya laini za simu za mkononi zinazotumika zina akaunti za kwa huduma za pesa kwa njia ya simu, huku miamala ikiongezeka kwa asilimia 76 ndani ya miaka mitatu.

Uwiano wa ukuaji wa akaunti za fedha kwa simu ulipita usajili wa laini za simu kati ya Machi 2026 na Machi mwaka huu. Hali hii ni dalili nzuri kuwa Tanzania iko kwenye njia sahihi kuelekea ujumuishi wa kifedha kwa wote.

| Desemba 2025 | Machi 2026 |
| --- | --- |
| Milioni 76.47 | Milioni 80.98 |


5.9%

*Akaunti za pesa kwa simu*

Laini za simu 52,813,930 na akaunti 32,720,180 za pesa kwa njia ya simu Machi 2021 ziliongezeka hadi 111,907,235 na 80,977,268 mtawalia Machi mwaka huu.

Miamala ya fedha kwa njia ya simu iliongezeka kutoka 421,094,958 Machi 2023 wakati kukiwa na akaunti 44,353,568 zilizotokana na laini 61,879,725 hadi miamala 742,751,361 Machi 2026. Miamala iliongezeka kwa asilimia 11.8 kati ya Desemba 2025 na Machi mwaka huu.

Akaunti za pesa za simu ni zile laini zenye akaunti za huduma ya pesa kwa njia ya simu ambazo zimesajili shughuli au zimetumika angalau mara moja katika miezi mitatu kabla ya ukusanyaji wa data za robo mwaka.





*Mgawanyo wa soko kwa kila mtoa huduma za pesa kwa simu*


Soko la fedha la simu la Tanzania lina viashirio mchanganyiko. Kuna ushindani mkubwa na hakuna mtoa huduma aliye na ukiritimba, ingawaje Vodacom, kupitia M-Pesa ina asilimia 40.97 ya soko. Watoa huduma wengine wenye hisa zao za soko kwenye mabano ni Yas/Mixx (31.02), Airtel Money (17.79), Halopesa (9.42), TTCL/T-pesa Azam Pesa (0.71) na Azam Pesa (0.09).

Azam Pesa inamiliki asilimia 0.09 ya soko lakini ilichangia asilimia 0.4 ya miamala yote mwezi Machi 2026. Kampuni hii ina huduma ya televisheni za kulipia ambazo zimepta umaarufu kwa chaneli za michezo.

Ingawa kulikuwa na akaunti 578,850 za pesa kwa katika mtandao wa TTCL mwezi Machi 2026, kampuni hiyo ilikuwa na miamala 192,345 tu katika kipindi hicho - asilimia 0.025 ya miamala ya makampuni yote sita yanayotoa huduma za pesa kwa simu.




*Mgawanyo wa soko kwa kila mtoa huduma kwa miamala iliyofanyika kwa simu*




*Mwenendo wa ukuaji wa miamala ya pesa kwa simu*

ISSN: 0856-8030



# Mikoa yafurika teknolojia ya 5G

TUsambazaji na uwekaji wa miundombinu ya teknolojia ya simu za mkononi kizazi cha tano (5G) Tanzania uliongezeka kwa asilimia 139 kati ya Juni 2024 na Machi mwaka huu, na mikoa yote ina angalau vituo vitatu.

Mikoa minne ambayo haikuwa na teknolojia hiyo kufikia Juni 2024 sasa ina angalau vituo vitatu. Idadi kwa kila mmoja kwenye mabano ni: Katavi (8), Lindi (7), Mtwara (6) na Kaskazini Pemba (3).


Vifaa vya 5G viliongezeka kutoka 754 hadi 1,804 kati ya Juni 2024 na Machi mwaka huu. Aidha viliongezeka kwa asilimia 44 kati ya Desemba 2025 na Machi 2026 - kutoka 1,255. Vimefungwa kwenye minara 10,084 ya mawasiliano ya simu za mkononi; ambapo vifaa vya kizazi cha pili (2G), cha tatu (3G), kizazi cha nne (4G) na 5G vimewekwa.

Five G iliingia Tanzania mwaka 2022. Teknolojia hii ina kasi ya juu zaidi ya data, inawezesha upakuaji wa haraka na unaweza kuunganisha vifaa vingi kwa wakati mmoja bila kuathiri ubora wa huduma na matumizi ya mtumiaji.

Mitandao ya 5G ina ucheleweshaji mdogo sana katika kutuma na kupokea data. Aidha yanawezesha mawasiliano baina ya vitu kwenye mandao wa intaneti.

Mawasiliano hayo ni kama vil yale ya mashine-kwa-mashine (M2M), ambapo vifaa hubadilishana data kiotomatiki na kufanya vitendo vingine bila kuingiliwa na binadamu.

Laini zinazowezesha M2M katika mitandao ya Tanzania ziliongezeka kwa asilimia 22 kati ya Juni 2024 na Machi 2026, kutoka 969,440 hadi 1,182,797.




*Mgawanyo wa Minara ya Mawasiliano kwa Teknolojia*



**4.7%**

*Kuongezeka laini za simu kwa mawasiliano ya watu (P2P) kunaonesha kuwa watu wengi zaidi wanapata huduma za mawasiliano ya simu.*



**4.4%**

*Kuongezeka laini za simu kwa mawasiliano kati ya mashine (M2M) kunaashiria kasi ya kuelekea mawasiliano kati ya vitu na huduma za kidijitali kiotomatiki.*

| Mwezi | Airtel | Halotel | TTCL | Vodacom | Yas | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 23,421,212 | 17,714,324 | 1,752,205 | 33,728,178 | 31,164,195 | **107,780,114** |
| Februari | 23,388,041 | 17,855,496 | 1,774,538 | 34,570,964 | 31,161,620 | **108,750,659** |
| Machi | 23,405,300 | 18,222,244 | 1,797,670 | 35,538,870 | 31,760,354 | **110,724,438** |

*Idadi ya laini za P2P kwa kila mtoa huduma*

| Mwezi | Airtel | Halotel | TTCL | Vodacom | Yas | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Januari | 339,354 | 88,020 | 3,461 | 628,330 | 83,385 | **1,142,550** |
| Februari | 344,353 | 90,520 | 3,467 | 637,262 | 85,419 | **1,161,021** |
| Machi | 346,794 | 93,520 | 4,023 | 648,069 | 90,391 | **1,182,797** |

*Idadi ya laini za M2M kwa kila mtoa huduma*

ISSN: 0856-8030




# Ulaghai mitandaoni wapungua lakini bado pasua kichwa

Matukio ya ulaghai kupitia mitandao ya simu za mkononi yaliyoripotiwa yamepungua kwa karibu asilimia 140 ndani ya miezi 30 lakini yamekithiri Rukwa na Morogoro.

Ingawaje matukio ya ulaghai yaliyoripotiwa yalipungua kutoka 23,328 Septemba 2023 hadi 9,816 Machi 2026, bado mikoa ya Rukwa na Morogoro inaongoza kwa sifa mbaya ya uhalifu huu. Hata hivyo matukio kwa Rukwa yamepungua kwa asilimia 114, kutoka 8,450 hadi 3,945 na Morogoro kwa asilimia 153 kutoka 6,571 mpaka 2,600.

Dar es Salaam, iliyokuwa na matukio 3,273 Septemba 2023 na Mbeya ambako matukio 1,905 yaliyoripotiwa inaonesha mabadiliko. Matukio 919 yaliripotiwa Dar es Salaam na 313 Mbeya Machi 2026. Mikoa yote ya Zanzibar haina matukio mengi, ambako kwa ujumla yaliripotiwa 15 tu Mschi mwaka huu, kutoka 43 kipindi tajwa.




*Idadi majaribio ya ulaghai kimkoa*

Uhalifu mitandaoni unahusisha wahalifu kuwalaghai watu kwa kuwapigia simu na kuwatumia ujumbe mfupi, yaani meseji za ulaghai na kuwataka watoe taarifa zinazohusu akaunti zao za pesa kwa simu au za kibenki, miamala, nywila na namba za siri. Matapeli wengine wanajidai wanahakiki namna za mtumiaji na kutaka taarifa zake. Hii inawawezesha wahalifu hao kuiba kwenye akaunti za pesa kwa simu, benki au za wakala wa huduma za pesa mtandao.


Ulaghai unahujumu mikakati ya serikali kuendeleza ushirikishaji wa wananchi kwenye mifumo ya kifedha na kujenga uchumi wa kidijiti. Vilevile unaathiri juhudi za Serikali kueneza huduma mbalimbali za jamii na za utawala kupitia mitandao.

Matukio yaliyoripotiwa kwenye mtandao wa TTCL yameongezeka kwa asilimia 98 kati ya Septemba 2023 na Machi 2026; kutoka 1,699 hadi 3,375. Mitandao mingine ilishuhudia kushuka.

Kwenye mtandao wa Airtel yamepungua kwa asilimia 460, kutoka 7,817 hadi 1,399. Hata hivyo yaliongezeka kwa asilimia 19 kati ya Desemba 2025 na Machi 2026.

Matukio na asilimia ya kushuka kwenye mabano mitandao mingine ni: Yas (Tigo), kutoka 8,608 hadi 3,375 – asilimi 155), Halotel (kutoka 1,167 hadi 500 – asilimia 133) na Vodacom (4,038 hadi 1,883 – asilimia 114).

Wachambuzi wanaelezea kupungua huku kuwa huenda kunatokana na uelewa watumiaji kuzingatia umuhimu wa kujilinda mitandaoni, kufuatia kampeni za TCRA za elimu kwa umma kuhusu usalama mitandaoni. Vilevile, hatua kali za kiusimamizi zimechangia. Hizi ni pamoja na kuwawajibisha watoa huduma ambao mitandao yao inakithiri kwa ulaghai.




*Asilimia ya matukio ya ulaghai kwa kila mtandao*

Kampeni ya TCRA inawataka waumiaji kujilinda mitandaoni kwa kutokutoa taarifa zao kwa watu wasiohusika. Pia wanatakiwa kuripoti matukio ya ulaghai kwa kutuma ujumbe kilaghai kwenye namba 15040 ambayo hailipiwi.

Elimu hiyo pia inasisitiza umakini wa watumiaji wanapofanya miamala ya kifedha. Aidha wanahimizwa kuhakiki namba zao za simu kupitia msimbo wa *106#.